# ***; KWANINI KUKU HAWATAGI MAYAI?***



Kuku hufugwa kwajili ya nyama na mayai, kama mfugaji atafuga kuku halafu hawatagi itakua hasara. Zipo sababu mbalimbali zinazosababisha kuku asitage. Mfugaji anatakiwa kuzitambua sababu hizi ili azitatue mapema.

1. ***Kuku kupata mwanga kidogo (siku kua fupi)***

Ili kuhakikisha kuku wanataga mayai kama kawaida, wanahitaji kiasi cha mwanga kwa masaa kati ya 14 hadi 16 haswa mwanga wa mchana. Kama siku

itakua fupi (masaa ya mwanga ni machache) kuku watapunguza kutaga na taratibu wataacha kabisa. Hiki ni kipindi cha kipupwe ambacho hua ni mwezi wa tisa, wa kumi na wa kumi na moja na kipindi cha baridi ambacho ni mwezi wa sita, wa saba na wa nane. Katika vipindi hivyo kuku hupunguza au kuacha kutaga kabisa katika maeneo mengi. Mfugaji anatakiwa aendelee kuwalisha kuku vizuri muda hu kwani kuku huirudishia afya miili yao na kujiandaa katika msimu mwingne wa utagaji.

Katika nchi zilizoendelea, wafugaji wanaweka taa (bulb) ambazo hutoa mwanga bandia ambao hufanya kazi kama mwanga wa jua hivyo kuku huendelea kutaga kama kawaida.

2. ***Umri***

Kuku wanataga kwanzia wakiwa na umri wa miezi mitano hadi miezi sita, wanaweza kuishi kwa miaka zaidi na kuendelea kutaga muda wote, japo baada ya miaka miwili hadi mitatu utagaji hupungua au kuisha kwa baadhi ya kuku. Baadhi ya kuku wametengenezwa kwajili

ya kutaga mayai mengi tu (layers) na hawa hutaga mwaka mzima lakini kuku wa kawaida (wa kienyeji) hutaga kwa misimu miwili tu kwa mwaka mzima. Hivyo mfugaji achague aina ya kuku anayotaka kufuga kutokana na uwezo wake. Pia kuku wa kienyeji kwajili ya kutaga wakifikisha umri wa miaka miwili au mitatu, basi wauzwe au wachinjwe kwani uwezo wao wa kutaga unakua umepungua au umeisha kabisa.

***3. Lishe duni***

Kuku anahitaji chakula chenye virutubisho vyote kwajili ya kuhakikisha

ukuaji wake na utagaji wa mayai. Ukosefu wa madini ya Calcium husababisha kupunguza kiasi cha mayai yanayotagwa au kuacha kutaga kabisa kwani Calcium inahusika katika kuandaa makasha ya mayai (Egg shell). Kama kuku atapewa vyakula duni mfano pumba pekee au makombo basi hatapata kiasi cha protini kinachohitajika kutengeneza yai.

Pia kama kuku atalishwa chakula chenye virutubisho vya wanga na mafuta mengi basi kuku atanenepa sana na kupunguza uwezo wa kutaga au kuku akitaga anakua anachanika sehemu za nyuma na hivyo

kusababisha mayai kua na kiasi cha damu.

4. ***Kukosekana kwa chakula na maji kwa ghafla***

Kama kuku watakosa au kupungukiwa na kiasi cha chakula au maji hata kwa muda mfupi basi kuku watakumbwa na upungufu wa utagaji au kuacha kutaga kabisa. Maji ndio virutubisho vya muhimu nzaidi kwa kuku zaidi ya vingine, na kuku ana uwezo wa kunywa maji hadi mara mbili ya chakula anachokula kwa siku. Wakati wa jua kuku hunywa maji hadi mara nne ya kiasi cha chakula

wanachopewa. Maji ya kuku yanatakiwa yawe masafi na salama ili kuepusha magonjwa.

5. ***Upungufu wa madini ( kwenye chakula)***

Madini ya Calcium ni muhimu kwa kuku wanaotaga kwani makasha ya mayai hutengenezwa na Calcium carbonate tumboni kwa kuku .Kuku akitoka katika hatuta ya kuku wanaokua kwenda katika hatua ya kuku wazazi wanahitaji kiasi kikubwa cha Calcium (hadi mara nne aya kiasi cha kawaida). Kama kuku watakosa madini ya Calcium, makasha ya mayai

yatakua mepesi hivyo mayai huvunjika kirahisi zaidi, mifupa ya kuku itakua dhaifu na wakati mwingine kuku hushindwa kusimama. Kuku wapewe makasha ya konokono, chokaa, chumvi, pia klorini (ambayo husaidia kuku katika mmen’genyo wa chakula)

Pia kuku wanahitaji vitamin D ambayo hupatikana katika mwanga wa jua.

6. ***Sumu;***

Vyakula vinavyovunda na kutengeneza sumu kama Mycotoxins au sumu ya

kwenye karanga au mashudu ya karanga
Aflatoxin hua na madhara kwenye afya ya kuku na utagaji mayai. Ni vizuri kuhakikisha chakula cha kuku kinatengenezwa na viambata vilivyokaushwa vizuri na kuhifadhiwa sehemu safi na kavu
Pia chumvi, ni nzuri kwa afya ya kuku lakini ikizidi katika chakula hua na madhara kwa kuku.

Pia kuku wasisogee karibu na dawa za shambani kama viuadudu, viuagugu, mbolea za viwandani na kemikali zingine

7. ***Kuzidi kwa joto***

Nyakati za joto kali kuku wanapunguza au kuacha kutaga kwani wanakua wanakula na kunywa maji zaidi ili kuifanya miili yao kuendelea kufanya kazi vizuri. Hakikisha kuku wana kivuli cha kutosha, madirisha makubwa na maji mengi ya kunywa wakati wa joto. Kiasi cha nishati kutoka kwenye chakula hutumika kukabiliana na kiasi cha joto kinachoongezeka.

8. ***Wadudu (wa ndani na nje ya mwili wa kuku)***

Chawa ni tatizo kwa kuku, viroboto,siafu na mchwa wanaweza kuua kabisa kuku kama banda la kuku halifanyiwi usafi mara kwa mara. Wadudu hawa huweza kuathiri ukuaji wa kuku na kupunguza utagaji wa mayai. Wadudu hawa huweza kudhibitiwa kwa kuafanya usafi mara kwa mara katika banda la kuku au kutumia dawa za wadudu wan je mfano Sevin Dudu dust. Minyoo pia hudhoofisha afya ya kuku na kuwafanya wapunguze

kutaga. Wape kuku dawa ya minyoo kila baada ya miezi mitatu

9. ***Magonjwa***

Kuku wanaweza kupata magonjwa kutoka katika mazingira yao. Kuku wagonjwa watajitenga na kuku wenzao, watapunguza kula chakula na kupunguza utagaji, Kuku wagonjwa wanatakiwa watengwe na kuku wenzao na wenzao na kutibiwa kwanza. Pia kuku wageni watengwe kwanza na kuwekewa chanjo ili wasiathiri kuku wazima. Magonjwa ya kuku kama kuhara (coccidiosis), mafua (

Infectious coryza) na mengineyo hua yanatibika ila magonjwa ya virusi kama Kideri, gumboro na ndui inabidi kuku wachanjwe mapema tangu wakiwa wadogo.

10. ***Kuku kutagia sehemu zilizojificha, na wizi wa mayai***

Wakati mwingine kuku hutagia maeneo ambayo sio rasmi hivyo kua rahisi kwa mayai kuibiwa na wezi au kupotea. Hi hutokea kwa kuku ambao huachiwa huru kuzurura hivyo hua ni hasara kwa mfugaji. Mayai mengine huliwa na

wanyama kama mbwa, paka na panya. Mayai mengine huliwa na kuku wenyewe ikiwa wanakosa baadhi ya virutubisho mfano Calcium

11. ***Mazingira ya kutagia yasiyo rafiki***
    Kuku wanahitaji viota vya kutagia vilivyo na mzunguko wa hewa wa kutosha na giza kidogo na iwe sehemu ya kujificha. Hi itasaidia kuku kua huru kujitenga na kuku wengine na kuzuia au kupunguza ulaji wa mayai. Sehemu ya kutagia inatakiwa iwe sehemu yenye matandazo ili kuku akitaga mayai yasichafuke au kuvunjika.

Kwa ushauri wa kitaalamu kuhusu ufugaji wa kuku;

**KWA MAHITAJI YA YA HUDUMA ZIFUATAZO**

- ✓ Vifaranga siku,wiki na mwezi aina

zote

- ✓ Mayai ya kuku ya kutotoleasha aina ya SASSO na KROILER
- ✓ Usimamamizi wa mradi wa ufugaji kuku
- ✓ Ushauri Zaidi juu ya ufugaji
- ✓ Uandishi wa mchanganuo biashara ya ufugaji ✓ Utafutaji wa masoko ya ufugaji.
- ✓ Vifaranga vya bata vya siku moja ✓ Mayai ya bata kwa ajili ya kutotolesha

**WASILIANA NAMI**

**KWA MAWASILIANO**

NAMBA ZA SIMU:

06564469991 Tigo

0620765518 Halotel

BARUA PEPE : Godwinmbwambo111